Katika uwanja wa kitaaluma, uprofesa ni ngazi ambayo wanataaluma wengi huitamani lakini ni wachache ambao huweza kuifikia. Hali hii inatokana na ukweli kwamba uprofesa anapewa mtu ambaye ametoa mchango mkubwa zaidi kitaaluma, ikiwa ni pamoja na kufanya tafiti mbalimbali na kutoa machapisho mengi. Profesa Mulokozi ni mmoja kati ya maprofesa wachache katika Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. Ametafiti na amechapisha sana. Pamoja na kupata uprofesa, Profesa Mulokozi ameonekana ni mwanataaluma wa pekee si tu katika utafiti na uchapishaji bali pia katika maisha ya kijamii. Haya yote hayakuwezekana kwa siku moja bali ni safari aliyoianza tangu utotoni ikibeba tajiriba na mitazamo mbalimbali. Sura hii inajumuisha historia kutoka vyanzo andishi, simulizi na maoni kutoka kwa watafitiwa mbalimbali kumhusu Profesa Mulokozi. Yumkini sura hii itawapa fununu wasomaji kuhusu sababu za Profesa Mulokozi kuwa kama alivyo na kufahamika kama anavyofahamika kitaaluma na kijamii